# OFISI YA RAIS TAMISEMI

# HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI

SHULE YA SEKONDARI SEDECO

S.L.P 176

MUGUMU- SERENGETI

05/12/2021

SIMU: 0752294852

KUMB. NA. SEDECO/J.I/VOL.1/3

JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………………………………

S.L.P…………………………………………………..

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SEDECO WILAYA YA SERENGETI MKOA WA MARA 2021**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza (I) katika Shule ya Sekondari SEDECO, mwaka 2021. Shule ya Sekondari SEDECO ni shule ya kutwa (DAY) ambayo ipo umbali wa KM17 kutoka makao makuu ya Wilaya ya Serengeti (Mugumu Mjini). Shule ipo katika kijiji cha BONCHUGU kata ya SEDECO kando ya HIFADHI YA SERENGETI.

Usafiri unaotumika zaidi ni Pikipiki au Gari

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021 ndani ya siku saba ili uanze masomo.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 SARE ZA SHULE**

**(a) Wavulana**

i. Suruali mbili DARK BLUE za heshima zenye marinda mawili mbele kitambaa kizito (model au suruali za kubana hazitakiwi)

ii. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi ya heshima (mashati mashati mafupi na yanayobana hayatakiwi)

iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba visiwe na visigino virefu au mabuti

iv. Mkanda mweusi wa ngozi

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI SEDECO
MUGUMU - SERENGETI

v. Soksi jozi mbili nyeusi
vi. Tai DAKI BLUE inayofanana na suruali
vii. Sweta la DAKI BLUE
viii. T- shirt (Flana ya manjano isiyo na maandishi yeyote)

**(b) Wasichana**

i. Sketi mbili za DAKI BLUE ziwe ndefu za kufika jicho la mguu, kitambaa kizito na marinda mapana
ii. Mashati mawili meupe mikono mifupi ya heshima (mashati mafupi na yanayobana hayatakiwi)
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika vyenye kamba visiwe na visigino virefu au buti (simpo au viatu vyenye urembo havitakiwi)
iv. Soksi jozi mbili nyeupe ndefu
v. Tai DAKI BLUE inayofanana na sketi
vi. Hijabu (shati refu na kitambaa chake cheupe na sketi ndefu inayogusa jicho la mguu na marinda mapana
vii. Sweta la DAKI BLUE
viii. T- shirt (Flana ya manjano isiyo na maandishi yeyote)

**TANBIHI:** Sare Zote hizi zitakaguliwa siku unaporipoti shuleni na mwanafunzi asiyekidhi sare hizo hatapokelewa

**2.2 DAFTARI**

Aje na madaftari 10 counter book Quire 2 au 3 kalamu za bluu au nyeusi, ufuto, penseli na mkebe (Mathematica set) na Rula

2.3 Ndevu, nywele ndefu ni marufuku, nyoa vizuri bila mitindo yeyote.

**2.4 SARE ZA MICHEZO**

Mwanafunzi awe na sare zifuatazo kwa ajili ya michezo shuleni

i. T-shirt (fulana ya manjano isiyo na maandishi yeyote na bukta ya bluu au jezi ya bluu)
ii. Raba au viatu vya michezo vigumu

**2.5 VIFAA VYA KUFANYIA USAFI**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja shuleni akiwa na vifaa vya usafi vifuatavyo

i. Jembe jipya 1 lenye mpini kwa wavulana tu
ii. Fyekeo 1 kwa wasichana tu
iii. Ndoo ya lita 10 moja kwa wote
iv. Ufagio wa chelewa 1 kwa wote

**2.6 REAM DOUBL A au A4 Moja kwa mwaka**

**2.7 FAIL 1**

## 3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya Elimu na Wizara ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa---- **TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti Shuleni.

### 3.1 Sheria na kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi , wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamiii kwa ujumla ni jambo la lazima
ii. Mahudhurio mazuri darasani na katika shughuli za ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya shule ni jambo la lazima
iii. Kushiriki kwa makini kufanya maandalizi ya jioni (Preparation)
iv. Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopangiwa
v. Kufafanua mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wowote wa ufafanuzi wako katika Shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya Shule
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unaotakiwa
viii. Kuzingatia ratiba ya Shule
ix. Kutunza mali za **UMMA**

3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa Shule

i. Wizi
ii. Uasherati na ushoga
iii. Ubakaji
iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine mirungi kubeli n.k
v. Kupiga au kupigana
vi. Kuharibu kwa makusudi Mali za Umma
vii. Kudharau Bendera ya Taifa
viii. Kuoa au kuolewa
ix. Kuwa mjamzito au kupata mimba au kusababisha mimba
x. Kutoa mimba (Abortion)
xi. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa Shule au watu.
xii. Kukataa adhabu kwa makusudi
xiii. Kuwa na simu ya mkononi

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

i. Medical Examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Form hii itakabidhiwa kwa mkuu wa Shule mara utakaporipoti Shuleni
ii. Form ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki migomo, fujo na makosa ya jinai
iii. Form ya mzazi kukiri au kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na Shule
iv. Cheti cha kuzaliwa.

5.0 Tafadhali zingatia kusoma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Mwanafunzi asiyetekeleza mahitaji, sare na maagizo aliyopewa hatapokelewa kwani jambo hili huleta usumbufu mwanafunzi anapofika shuleni bila kukamilisha mahitaji aliyoagizwa.

# SHULE YA SEKONDARI SEDECO

1. **AHADI YA MZAZI / MLEZI KUHUSU KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEZO MENGINE**

Mimi Bw/ Bi_____________________________________________ambaye ni
(Mhusika)_____________________________________________wa mwanafunzi
(Taja Jina lake) _____________________________________________baaada ya
kusoma maagizo yote ya kujiunga na Shule hii na kuyaelewa Vizuri nina ahidi kukubaliana na Sheria, Kanuni na Maelezo mengine yote yaliyotolewa na Shule kuzingatia waraka wa Elimu Na 5 wa mwaka 2015 kama Mzazi /Mlezi nitayatekeleza majukumu yangu yote katika muda mwaafaka ili mtoto aweze kusoma ipasavyo.

Sahihi ya Mzazi/
Mlezi____________________________Tarehe_________________

2. **AHADI YA MWANAFUNZI YA KUKUBALI KUFUATA MAAGIZO YOTE YA SHULE KAMA MWANAFUNZI**

Mimi _____________________________________________baada ya kusoma maagizo ya kujiunga na Shule na Sheria za Shule. Nina ahidi kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zote za shule kwa kipindi chote nitakapokuwa mwanafunzi na kutoshiriki migomo, fujo na makosa ya Jinai. Nipo tayari kuadhibiwa kwa mujibu wa Sheria na taratibu za Shule endapo nitabainika nimekiuka kanuni na Sheria za Shule.

Sahihi ya
mwanafunzi________________________________Tarehe_______________

Karibuni sana katika Shule hii ya SEDECO sekondari

BARIKI M. KABUJE
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI SEDECO
MUGUMU-SERENGETI

## SHULE YA SEKONDARI SEDECO
## TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

1. Majina kamili ya mwanafunzi________________________________________
   Jinsia_____ Dini_________________________

2. Mwaka wa kuzaliwa Tar___/___/_______

3. Majina ya wazazi/ Walezi
   i. Baba____________________________________yu hai (Ndiyo/Hapana)
   ii. Mama _________________________________yu hai (Ndiyo/Hapana)
   iii. Mlezi _______________________________________

4. Anwani yako ya Makazi
   Kijiji ____________________________S. L. P ____________________________
   Mji______________________________Simu____________________________

5. Jamaa wa karibu
   i. ______________________Uhusiano__________Simu _____________
   ii. ______________________Uhusiano __________Simu _____________
   iii. ______________________Uhusiano__________Simu_____________

   Jina la mwanafunzi __________________________________________

   Sahihi ______________________Tarehe______________________

**FOMU HII IKABIDHIWE KWA MKUU WA SHULE SIKU YA KURIPOTI**

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

FROM; THE HEADMASTER
SEDECO SECONDARY SCHOOL
MUGUMU – SERENGETI
DATE ……………………………………

**PART A**
**TO THE MEDICAL OFFICER**

……………………………………
……………………………………
……………………………………
……………………………………
……………………………………

**REF: MR/MRS/MISS**

…………………………………………………………………………………………………

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness.
The examination should include the following categories (i-iii) each category of which will render the applicant in eligible (category iii) will also render a girl's candidate in eligible being a student.

a) Eye sight ……………………………………………………………………………
b) Hearing ………………………………………………………………………………
c) Speech ………………………………………………………………………………
d) Limbs …………………………………………………………………………………
e) Venereal disease ……………………………………………………………………
f) Leprosy ………………………………………………………………………………
g) Peptic ulcers …………………………………………………………………………
h) Epilepsy ………………………………………………………………………………
i) Tuberculosis …………………………………………………………………………
j) Neuroses………………………………………………………………………………
k) Other serious disease ………………………………………………………………
l) Pregnancy ……………………………………………………………………………
m) Mental and physical fitness ………………………………………………………

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

I have examine the above named and consider that he/ she is "physical fit", unfit a full time being student.

Date ……………………………………… Signature ……………………………
Station …………………………………… Signature ……………………………

**'DELETE AS NECESSARY '**